**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

SHULE YA SEKONDARI KIZIGO


Email: kizigoss@gmail.com

S.L. P 252, Simu: Mkuu wa Shule 0767 474 171 / 0784 474 171

MANYONI- SINGIDA


Mwanafunzi…………………………………………

…………………………………….

S.L.P……………….

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIZIGO WILAYA YA MANYONI KIDATO CHA TANO MWAKA**

1.0. Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga Kidato cha …………. Tahasusi ya………..katika shule ya Sekondari KIZIGO Mwaka………………………………………………………….

**2.0. MAHALI SHULE ILIKO**

Shule hii iko umbali wa kilometa arobaini na nne (44) Kutoka Manyoni mjini. Shule itafunguliwa tarehe itakayotangazwa na Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI

**3.0. JINSI YA KUFIKA SHULENI**

Fika kituo kikuu cha mabasi cha Manyoni Mjini maarufu kama Lami upande mabasi yanayokwenda Sanza ama Sasilo ama Heka na Utashushiwa Kizigo Sekondari. Nauli ya basi ni Tsh 5000/

**3.1. Mambo muhimu ya kuzingatia.**

3.1.1. Sare ya shule na mahitaji ya shule ni:

i. Sketi mbili (2) za kijivu iliyokolea zenye rinda box la V mbele. Iwe ndefu yenye kuvuka magoti (Kitambaa cha suti Esteem Na 1)
ii. Sweta za Kijivu zenye shingo ya V.
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu kwa wote.
iv. Soksi nyeupe ndefu Jozi 3
v. Kwa Waislamu wanaovaa Hijab, iwe nyeupe isiyo na marembo
vi. Mashati ya blue bahari ya cotton/tetron ya mikono mirefu kwa wote

**3.2 SARE ZA SHULE ZA KUSHINDIA**

Nguo za kushindia (shamba dress) ni magauni mawili(2) ya DARK BLUE ya Cotton au kitambaa cha suti kisichong'aa mshono wa solo mikono mafupi

**3.3 SARE ZA MICHEZO**

**i.** Tshirt Rangi ya light blue zenye colar (Form six) ukipenda unaweza kuzipata shuleni kwa Tsh 15,000/ Pea moja

ii. Track suit za rangi ya Kijivu zenye stripes 2 pembeni

iii. Sketi fupi rangi ya blue Kitambaa cha sukarisukari , Pia ajae na raba nyeusi jozi 1 na soksi nyeusi jozi 2

**4.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI**

i. Madaftari Kaunta quire 3 yawe 10, madaftari 10 aina ya Msomi

ii. Ream mbili (2) (A4) kwa mwaka;

i. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Rejea kiambata "B"hapo chini). Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

ii. Scientific Calculator

iii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pinki, blanket 1, foronya ya pinki, mto 1, godoro 1(size 2½"x6"), chandarua 1(4"x6")

iv. rangi nyeupe.

v. Passport size tatu (3)

vi. Nguo za ndani za kutosha na taulo za kike

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na ndoo 1 ya Lita 20

ix. Kwanja 1, jembe 1, mifagio 2 wa ndani soft broom na wa nje chelewa (brash ngumu) hard broom kwa wanafunzi wa tahasusi ya PCB

x. Sanduku la bati ( Tranka)

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI

KIZIGO

JANETH R.

LUBASI

MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
KIZIGO SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 252
MANYONI

## 5.0 MICHANGO MBALIMBALI YA SHULE

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| 2 | Tahadhari | 5000 |
| 3 | Nembo | 5000 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5000 |
| | **JUMLA** | **80,000** |

- **Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule 50701100062 Jina la akaunti KIZIGO SEC SCHOOL RECURENT ACCOUNT (NMB)**
- **Kwa mwanafunzi asiye na BIMA ya afya,akatiwe Bima ya afya au aje na Tsh 6000/= (cash), kwa ajili ya kumkatia Bima ya afya ili kuepuka usumbufu pindi mwanafunzi atakapo ugua(muhimu).**

**N.B: Mwanafunzi aje na risiti ya michango original na aikabidhi kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti.**

## 6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 6.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo Asuhihi na ya usiku (Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**7. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI**

**KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;
viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xii. xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiii. xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xiv. xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**8.0 VIAMBATANISHO FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;(Kiambata “B”)
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na
iii. makosa ya jinai;(Kiambata “C”)
iv. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; (Kiambata “E”) na iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**9.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

” **NIDHAMU NA BIDII HULETA MAFANIKIO**”

KIAMBATA
"A"
ARTICLE I. TAALUMA: -

Kwa kuwa shule ina uhaba wa vitabu, inashauriwa mwanafunzi aje na vitabu vitakavyomsaidia kwa masomo husika kati ya vilivyoorodheshwa hapa chini:- ARTICLE II. I. VITABU VYA KEMIA: -

1. Jain s.k (2006) Conceptual Chemistry XI ,4th edition. Chand, New delhi India

2. Ngaiza lusima (2014) Atomic Structure and Bonding. Hopegen company ltd. Dar es salaam. Tanzania

3. Ngaiza lusima (2014) Physical Chemistry. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania

4. Ngaiza lusima (2014) Inorganic Chemistry. Hopegen Company Ltd. Dar Es salaam. Tanzania

5. Ngaiza lusima (2014) Environmental and Soil Chemistry. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) Calculations for A-level chemistry.

II. VITABU VYA BIOLOJIA: -
1. Gleen and Toole (1999). Understanding Biology 4th Edition.Stanlye Thomes LTD UK.
2. Kent M. (2013). Advanced Biology.Oxford University Press LTD 2nd Edition
3. Aggarwal S. (2017). A text book of CBSE.Biology for Class XI.Nijra Publishers and Printers PVT.LTD
4. Verma P. S and Pandey BP (2012). S. Chands Biology for class VI.Chand and Company LTD.New
5. Delh
6. 5 Verma P. S and Pandey BP (2012). S. Chands Biology for class VII.Chand and Company LTD.New Delh
7. 6 Taylor etal (1997) Biological Science.3rd Edition, Cambridge university Press LTD.
8. 7 T.I.E (2019) Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Six, Dar es salaam, T.I.E
9. 8 T.I.E (2019) Biology for Advanced Level Secondary School.Student's

ARTICLE V. VI. VITABU VYA
PHYSICS: -
1. 1.Mehta, R. and V. K Mehta (2009) "Principles of Physics for Class XI" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.
2. Nelcon, M and P. Parker (1995) "Advanced level Physics'' 07thEdition, London, Heinmann Educational books.
3. 3. TIE (2019) "Physics for Advanced Level Secondary Schools, Form Five, Dar es salaam, TIE.

XII. GENERAL
STUDIES: -

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M.5th Edition (2019) Understanding Advanced Level General Studies, Dar es salaam, Mikumi Publishers.
2. Tanzania Institute of Education (2010), General Studies for SecondaryEducation, Dar es Salaam, T.I.E

KIAMBATA
'B'

KIZIGO SECONDARY SCHOOL

ARTICLE VIII. MEDICAL
EXAMINATION FORM

To be completed by a medical officer in respect to all form of entrants
Student's full name …………………………………………………………………………

Age ……… Years ……… Sex ………………….

Blood count (red and whites) ………………………………………………………………
Stool examination ………………………… Urine analysis
Syphilis and other venereal diseases test ………………………………………………
T.B test ……………………………………
EyeTest…………………………………………
……………………………
Ears……………………………………………
………………………………..
Abdomen………………………………………
………………
Urine for plant ……………………………………
Test for pregnancy…………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotents (e.g., arms, legs etc) infections, chronic or family diseases etc
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education
Station ………………………………………………Signature………………………
Date………………………………………………designation……………………

**KIAMBATA ‘C’**

**SHULE YA SEKONDARI KIZIGO**

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII: -

ARTICLE IX. A. WAZAZI/WALEZI

1. Jina la Baba …………………………………………………. Hai/Si hai.
2. Jina la Mama ………………………………………………. Hai/ Si hai.
3. Kama Baba si hai jina la mlezi ni …………………………………………………………
4. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………
5. Anwani ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………
6. Uraia wa wazazi

• Baba Mtanzania/Si Mtanzani.
• Mama Mtanzania/ Si Mtanzania.

7. Wakati wa likizo mtoto/Mwanafunzi anatakiwa arudi nyumbani kwao alikotoka ambako ni………………………………………………………………………
8. Jina la mtu aendako ………………………………………………………
9. Uhusiano na mtoto/mwanafunzi…………………………………………… SAHIHI YA BABA/MLEZI…………………………TAREHE …………………. SAHIHI YA MWANAFUNZI …………………………TAREHE ………………… N.B. KILA

MWANAFUNZI ANAPOKUJA AJE NA NAKALA YA CHETI CHAKE CHA KUZALIWA NA NAKALA YA KADI YA NIDA YA MZAZI, KAMA MZAZI HANA KADI YA NIDA MWANAFUNZI AJE NA NAMBA YA NIDA. AIDHA MWANAFUNZI MWENYE KADI YA BIMA YA AFYA AJE NY

**KIAMBATA "D"**

**SHULE YA SEKONDARI KIZIGO**

# ARTICLE X. FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi ……………………………………………………………………………… nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa

kwangu kuingia shule ya Sekondari Kizigo ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu nafasi ni chache. Hivyo nakubali kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana Mwanza.

Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Sekondari Kizigo na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

(i).Tahasusi………. (ii). Uraia…………………… (iii). Kabila……………………

(iv).Dini……………………………Dhehebu…………………………………………

.

(vi). Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………

(Vii). Mahali ulipozaliwa: Kitongoji/mtaa……………………….……Kijiji………………… Kata……………………………………...Tarafa………………………… Wilaya/Mji…………………………….…… Mkao…………………………

(viii). Taarifa za Shule ulizosoma: -
Msingi…………………………………………Sekondari……………………………

Tarehe…………………………… Sahihi ya mwanafunzi………………………...

Mimi Mzazi/ Mlezi………………………………………………………,Nmeshuhudia mtoto wangu ……………………………………….. akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo, ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea binti yangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe…………………………………Sahihi ya Mzazi/Mlezi…………………